



TAARIFA KWA UMMA

KONGAMANO KUHUSU HALI YA UCHUMI NA SIASA NCHINI TANZANIA

Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kinapenda kuwaalika wanajumuiya wote wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na umma kwa ujumla kushiriki katika Kongamano maalum lililoandaliwa mahsusi kufanya tafakuri ya kisomi kutathmini miaka mitatu ya utendaji wa Serikali ya Awamu ya Tano na kutoa mapendekezo yenye lengo la kuboresha utendaji wa Serikali katika kuleta maendeleo kwa Wananchi. Ikumbukwe kuwa, mnamo tarehe 5 Novemba 2018 Serikali ya Awamu ya Tano chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itatimiza miaka mitatu tangu kuingia madarakani. Katika kipindi hiki Serikali imechukua hatua mbalimbali za kuboresha uchumi, huduma za jamii, upatikanaji wa nishati, miundombinu, kuinua sekta ya viwanda, kudhibiti matumizi mabaya ya rasilimali za umma, kuongeza nidhamu katika utumishi wa umma, kupambana na rushwa, na kuongeza uwajibikaji.

Kongamano hili litafanyika siku ya Alhamisi tarehe **1 Novemba 2018** kuanzia saa 3:00 asubuhi mpaka saa 6:30 mchana katika ukumbi wa Nkrumah, Kampasi ya Mwalimu Julius Nyerere, Mlimani. Mada kuu ya Kongamano hili ni **“Hali ya Uchumi na Siasa Nchini Tanzania”**.

Wazungumzaji wakuu katika Kongamano hili watakuwa ni:

1. Profesa Humphrey Moshi, Idara ya Uchumi, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam
2. Profesa Hudson Nkotagu, Idara ya Jiolojia, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam
3. Profesa Martha Qorro, Idara ya Lugha za Kigeni na Isimu, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam
4. Profesa Kitila Mkumbo, Katibu Mkuu, Wizara ya Maji
5. Profesa Rwekaza Mukandala, Idara ya Sayansi ya Siasa na Utawala, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

Washiriki wa Kongamano hili watakuwa wanataaluma, watunga sera, viongozi wa serikali, wadau wa maendeleo, mabalozi, viongozi wa kisiasa, vyama vya kiraia, na wananchi wote kwa ujumla. **Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli atakua Mshiriki Maalum wa Kongamano hili**. Pia Kongamano linatarajiwa kurushwa mubashara katika baadhi ya vituo vya televisheni na kwenye mitandao ya kijamii.

Imetolewa na

Profesa William A. L. Anangisye
Makamu Mkuu wa Chuo

CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM



RATIBA YA KONGAMANO KUHUSU HALI YA UCHUMI NA SIASA NCHINI TANZANIA

Ukumbi wa Nkrumah, Tarehe 1 Novemba, Saa 3:00 Asubuhi

MUDA	TUKIO	MHUSIKA
02:00 – 03:00	Kuwasili na Kujisajili	Kamati ya Maandalizi
03:00 - 03:10	Wimbo wa Taifa	Bendi ya JWTZ
	Neno la Ukaribisho	Makamu Mkuu wa Chuo Prof. William A. L. Anangisye
	Burudani	Bendi ya JWTZ
03:10– 03:13	Kumtambulisha Mtoa Mada wa Kwanza	Rasi, Chuo Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam (DUCE) Prof. Bernadeta Killian
03:13 – 03:28	Mada ya Kwanza “Hali ya Uchumi na Maendeleo ya Viwanda”	Prof. Humphrey Moshi
03:28 – 03:31	Kumtambulisha Mtoa Mada wa Pili	Naibu Makamu Mkuu wa Chuo – Utawala Prof. David Mfinanga
03:31 – 03:46	Mada ya Pili “Nishati na Miundombinu”	Prof. Hudson Nkotagu
03:46 – 03:49	Kumtambulisha Mtoa Mada wa Tatu	Mkurugenzi wa Taasisi ya Sayansi za Bahari Zanzibar (IMS) Dr. Margareth S. Kyewalyanga
03:49 – 04:03	Mada ya Tatu “Lugha na Maendeleo”	Prof. Martha Qorro
04:03 – 04:06	Kumtambulisha Mtoa Mada wa Nne	Rasi Chuo Kishiriki cha Elimu Mkwawa (MUCE) Prof. Esther Dungumaro
04:06 – 04:21	Mada ya Nne “Huduma za Jamii”	Prof. Kitila Mkumbo
04:21 – 04:24	Kumtambulisha Mtoa Mada wa Tano	Naibu Makamu Mkuu wa Chuo – Utafiti Prof. Cuthbert Kimambo
04:24 – 04:39	Mada ya Tano “Hali ya Siasa na Utawala”	Prof. Rwekaza Mukandala
04:39 – 04:45	Burudani	Bendi ya JWTZ
04:45 – 06:20	Majadiliano	Mwenyekiti Prof. William A. L. Anangisye
	Neno la Shukrani	Rasi wa Ndaki ya Sayansi za Jamii Prof. Alexander Makulilo
06:20 – 06:25	Picha za Pamoja	Amidi wa Kongamano
06:25 – 06:30		
06:30	Mwisho	Wote